NORTHERN TERRITORY GOVERNMENT

DEPARTMENT OF HEALTH

Uchaguzi wa ujauzito kwa wanawake katika Wilaya ya Kaskazini

Nimejamiana bila kinga – nifanye nini?

Ikiwa umejamiana bila kinga au mpango wa uzazi umeshindwa na hutaki kupata mimba, labda utaweza kutumia kidonge cha dharura cha kuzuia uzazi. Vidonge vya dharura vya kuzuia uzazi VINAHITAJI KUMEZWA KATIKA SIKU TANO (5) baada ya kujamiana bila kinga na vinapatikana kutoka famasia nyingi baada ya kupata ushauri wa mfamasia. Si lazima kuwa agizo la madawa. Ikiwa huishi katika jamii ya porini vinapatikana kawaida kutoka kliniki ya afya ya eneo lako.

Nafikiri nina mimba

Wanawake wengi wanapata mimba ambao hawakupangiliwa kwa wakati wengine katika maisha yao. Kuhakikisha kwamba una mimba waweza:

- Tumia kipimo cha uzazi cha nyumbani kutoka famasia au duka kuu
- Umwone daktari yako anayeweza kufanya kipimo cha kojo au dawa
- Umwone Ustawi wa Kupanga Uzazi kwa NT (pale Darwin)
- Enda kwa kliniki cha eneo lako

Uzazi bila mpango

Wanawake wengi wanapata mimba bila mpango au bila kutazamia kwa wakati fulani katika maisha yao. Kuna uzazi bila kupangiliwa karibu 200,000 kila mwaka nchini Australia.
Kila mwanamke ana haki ya kuamua uamuzi wake mwenyewe na kijitabu hiki kitakusaidia kuelewa uchaguzi wako na kukusaidia kuamua uamuzi.

Mimba umepangiliwa lakini kuna shida na ujauzito

Unaweza kuwa na mimba iliyopangiliwa lakini unagundua kuna shida. Hii inaweza kuwa muda ya kuhangaika sana na utahitaji habari kuhusu uzazi wako kutoka daktari yako na wataalamu wengine na kupata maelezo yao kuhusu matokeo ya vipimo vyovyote. Ndipo waweza kuzungumza uchaguzi wako wote na daktari yako, familia yako na wengine.

Kupata msaada

Labda utataka au hutataka kuongea kuhusu ujauzito wako lakini inaweza kufaa kuongea na mtu ambaye unaamini anayeweza kutoa maelezo bila baguzi. Kuna tovuti nyingine za kufaa zilizoorodhesha kwa mwisho wa kijitabu hiki zinazoweza kutoa habari na kukusaidia kuamua uamuzi.

Uchaguzi Tatu

Wakati unapopata tatizo bila mpango au kutazamia na ujauzito kuna uchaguzi tatu:

1. Endelea na mimba na uwe mzazi wake
2. Endelea na ujauzito na panga kubadilisha mtoto
3. Toa mimba (pia inaitwa abortion)

1. Endelea na mimba na kuwa mzazi

Kuchagua kuwa mzazi ni uamuzi wa kubadilisha maisha. Ukichagua kuendelea na ujauzito wako, panga miradi na daktari yako atakayekusaidia kupanga hatua zingine.

2. Kubadilisha mtoto

Kubadilisha mtoto inatokea kama haki na majukumu ya kisheria kwa kulea mtoto zinabadilishwa kwa kudumu kutoka wa/mzazi wa kuzaliwa kwenda wazazi wa kubadilisha mtoto.
Kituo cha Kubadilisha Mtoto cha Wilaya ya Kaskazini ni sehemu ya Familia ya Wilaya na kina jukumu kwa mipango ya kubadilisha mtoto katika Wilaya ya Kaskasini. Ikiwa unataka kufikiria kufanya mpango wa kubadilisha mtoto umwasiliane na Kituo cha Kubadilisha Mtoto.

Kituo cha Kubadilisha Mtoto - Familia ya Wilaya
Simu: (08) 8922 5519
Baruapepe: TF.Adoptions@nt.gov.au
Anwani ya Posta: PO Box 40596 Casuarina NT 0800

Kituo hiki kitapanga miradi kwa wewe kuzungumza uchaguzi wako na utaratibu wa kubadilisha mtoto.

3. Kutoa Mimba (abortion)

Kutoa mimba ni tiba ya kawaida kidogo nchini Australia. Karibia 1 wa wanawake 3 nchini Australia anatoa mimba angalau mara moja katika maisha yake na kutoa mimba kwingi kunatokea katika wiki 14 za kwanza ya ujauzito. Kuna aina kuu mbili ya kutoa mimba:

Kutoa Mimba Mapema kwa Tiba

- Hii inajulikana kama tiba ya uganga ya hatari ndogo
- Ujauzito wako uwe chini ya wiki tisa (au siku 63)
- Utamwona daktari aliyepata mafunzo ya kutoa madawa kwa kutoa mimba
- Viwango vya mafaniko kwa kutoa mimba mapema kwa tiba ni hadi 98% katika wiki 9 za kwanza za ujauzito lakini mara adimu maendeleo hayaisha na labda utahitaji tiba ya kupasua ya tofauti.
- Habari zaidi kuhusu aina hii ya kutoa mimba zimo kijitabu kingine *"Kutoa Mimba katika Wilaya ya Kaskazini"*

Kutoa Mimba kwa Kupasua

- Kutoa mimba kwa kupasua (chini wiki 14) ni tiba ya hatari ndogo kufanyiwa hospitalini au kupasua zahanati ya siku
- Unapewa dawa ya nusukaputi mwilini na tiba kawaida inachukua dakika 10-15
- Kawaida unaweza kwenda nyumbani siku ileile
- Utapata maumivu na kutoa damu baada ya kutoa mimba kwa kupasua na utahitaji kuwa na mtu wa kukusaidia kukusindikiza nyumbani kutoka hospitali
- Kuna hatari kila wakati kuhusiana na upasuaji au dawa ya nusukaputi. Habari zaidi kuhusu aina hii ya kutoa mimba zimo kijitabu kingine *"Kutoa Mimba katika Wilaya ya Kaskazini"*

Kufanya nini ukiona unataka kutoa mimba?

- Zungumza na daktari, muuguzi au mweledi wa afya wako kuhusu uchaguzi wako kwa kutoa mimba
- Soma kijitabu cha *"Kutoa Mimba katika Wilaya ya Kaskazini"*

Maelezo kupitia mtandaoni

Ufahamu kwamba huduma zingine zinaweza kutoa habari zenye baguzi kuhusu uchaguzi wa mimba. Utahitaji kufikiria habari wewe mwenyewe na kuchagua nini ni nzuri sana kwako.

Hapo ni tovuti zingine zinazoweza kukusaidia kuamua uamuzi kuhusu mimba bila mpango.

Watoto kwa Uchaguzi ni huduma ya habari, mapendekezo na ushauri wa kipaumbele cha wanawake, pale Queensland ambayo inakubali uchaguzi, bila-kutawala na bila-baguzi. - **kwa wanawake bonyeza hapa** - **kwa wanawake vijana bonyeza hapa** **Kuhakikisha habari unazozisoma zinaaminifu na hazibaguzi bonyeza hapa**
Shine Australia ni Shirika la Mpango wa Uzazi la Australia Kusini na zinapatikana habari zifuatazo kwa tovuti yao Habari za Uchaguzi wa Mimba
Mpango wa Uzazi Tasmania ina tovuti na habari za uchaguzi wa ujauzito na unaweza kupata kwa kubonyeza hapa.

Kanusho

Habari katika hati hii imetolea kwa malengo ya kutoa habari na elimu tu. NT Afya imeonyesha uangalifu sana kuhakikisha kwamba habari ni sahihi na za sasa-hivi kwa wakati wa kuchapisha. Watu ambao wana wasiwasi kuhusu swala yoyote ya uzazi au kigono cha kibinafsi wanashauriliwa kutafuta ushauri na msaada kutoka utoaji wa utunzaji wa afya.